

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

SimuNa: +255 (028) 2227148  
Nukushi: +255 (028) 2227140



Halmashauri ya Wilaya  
S.L.P 20  
**KARAGWE**

Barua Pepe: [ded@karagwedgec.go.tz](mailto:ded@karagwedgec.go.tz)  
[utumishi@karagwedgec.go.tz](mailto:utumishi@karagwedgec.go.tz)

*Unapo jibu tafadhali taja:*

Kumb. Na. KGR/HWK/T.10/VOL.XVIII/103

22/10/2021

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI (MTENDAJI WA  
KIJIFI DARAJA LA III) NAFASI (1)**

Halmashauri ya Wilaya Karagwe imepata kibali cha Ajira kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kuitia Barua yenye Kumb. Na. FA.170/368/01 "B"/110 ya tarehe 13 Septemba, 2021. Kuitia barua hiyo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe anapenda kuwatangazia Wananchi wote wenye sifa kuomba ili kujaza nafasi husika.

**SIFA ZA MWOMBAJI:-**

Mwombaji awe ni mwenye ufaulu wa Elimu ya Kidato cha Nne(IV) au Sita (VI) aliye hitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya sanaa kutoka chuo cha serikali za mitaa Hombolo au Chuo chochote kinachotambuliwa na serikali.

- i. Awe na umri wa kuanzia miaka 18 hadi 45
- ii. Awe ni raia wa Tanzania
- iii. Awe na akili timamu.
- iv. Awe hajawahi kushitakiwa na kufungwa kwa kosa la jinai
- v. Mwombaji ambatanishe cheti cha kuzaliwa (Birth Certificate).
- vi. Mwombaji ambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (detailed CV) yenye anwani na namba za simu pamoja na wadhamini (referees) watatu(3) wa kuaminika.

- vii. Maombi yote yaambatane na barua ya maombi, nakala ya vyeti vya taaluma, nakala ya vyeti vya kidato cha Nne au Sita kwa waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
- viii. Testimonials, Provisional results, statement of results, hati ya matokeo ya kidato cha Nne na Sita
- ix. Waombaji waambatanishe picha mbili za passport size za hivi karibuni.
- x. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi
- xi. Hakikisha una kitambulisho cha NIDA au Namba ya Utambulisho wa Uraia

## **MSAHARA**

- i) Mshahara kwa mwezi TGS B1

## **KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIJI**

- i) Afisa masuuli na Mtendaji Mkuu wa Kijiji
- ii) Kusimamia ulinzi na usalama wa Raia na mali zao. Kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa utawala bora katika kijiji.
- iii) Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kijiji.
- iv) Katibu wa mikutano na kamati zote za Halmashauri ya kijiji.
- v) Kujibu na kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa umaskini, njaa na kuongeza uzalishaji wa mali.
- vi) Kiongozi wa wakuu wa vitengo katika Kijiji.

- vii) Kuibua vyanzo vya mapato na kusimamia ukusanyaji wa mapato ya kijiji.
- viii) Kuandaa na kutunza Rejesta ya wakazi wote wa kijiji.
- ix) Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata na Mkurugenzi Mtendaji.
- x) Mwasilishaji taarifa zote muhimu za kijiji kwa Afisa Mtendaji wa Kata (WEO)
- xi) Kupanga na kuhakikisha kupitishwa ratiba za vikao vya mkutano mkuu na halmashauri ya kijiji.
- xii) Mfutiliaji wa miradi ya kijiji na kutoa taarifa kwenye Halmashauri ya kijiji .

**NB:** Maombi yote yatumwe kwa:-

Mkurugenzi Mtendaji  
Halmashauri ya Wilaya,  
S.L.P 20  
**KARAGWE.**

*Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 04/11/2021 Saa 9:30 Alasiri*

Imetolewa na:

  
A.A. Nkindwa.

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI**

**MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
KARAGWE**